

## **Sekta ya Kilimo, Mifugo na Umwagiliaji**

### **A.kilimo na umwagiliaji**

- ❖ Asilimia 80 ya wakazi wa Wilaya ya Ileje hutegemea kilimo kama nyenzo kuu ya uzalishaji mali. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, alizeti, mihogo, mpunga, viazi vitamu, viazi mvirigo, maharage, karanga, soya na ndizi.
- ❖ Zao kuu la biashara ni Kahawa likifuatiwa na pareto, mazao mengine ni pamoja na iliki, alizeti, kokoa,ngano na parachichi.
- ❖ Wilaya ya Ileje ina jumla ya mashamba darasa 36 ya mazao ya chakula na biashara yaliyopo vijijini.
- ❖ Aidha, wilaya ina eneo linalofaa kwa Kilimo lipatalo hekta 101,600 kati ya hilo eneo linalolimwa kwa sasa ni Hekta **80,110** sawa na 78.85% ya eneo lote linalofaa kwa kilimo.

### **Hali ya Chakula**

- ❖ Wilaya ya Ileje imefanikiwa kuwafikia wakulima zaidi ya 90% kati ya wakulima waliopo na kuwapatia elimu na ujuzi wa kitaalamu kuhusu mbinu za kilimo bora cha mazao ya biashara na chakula.
- ❖ Kufuatia usimamizi wa kitaalamu na ushirikishaji wa wakulima uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka hadi kufikia tani **348,211** katika msimu ulioishia Juni 2022 kutoka tani **305,128** zilizozalishwa katika msimu uliopita wa mwaka 2021(Juni) na kuifanya Wilaya yetu kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya kuuza.